**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI MUGANGO**

**Shule ya Sekondari Mugango**

**S.L.P:1355, MUSOMA**

**.............**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..................................................**
**S.L.P ...............................**

Yah**:** **<u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUGANGO HALMASHAURI YA MUSOMA MKOA WA MARA MWAKA...............</u>**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya **EGM/CBG**.

Shule ya Sekondari Mugango ipo umbali wa Kilometa 25 Kusini mwa Mji wa Musoma.

Usafiri wa basi kutoka mjini Musoma unapatikana katika kituo cha Mabasi cha zamani nauli ni shilingi 3,000 kwa mabasi ya kwenda Majita kupitia barabara ya Majita road.. Teremkia kituo cha Mugango Sekondari.

Muhula wa masomo unaanza tarehe .................. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..............,,, saa 02:00 asubuhi siku ya Jumatatu, Ofisi ya Makamu wa mkuu wa shule itakuwa wazi kwa mapokezi na usajili ukiwa na vifaa kama ulivyoagizwa kwenye form hii.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule kwa wasichana

i. Sketi mbili za bluu bahari zinazovuka magoti zikiwa na mshono wa rinda box na mfuko mmoja.
ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
v. Soksi jozi mbili nyeupe.
vi. Sweta rangi ya dark bluu yenye V shingoni.
vii. T-shirt mbili za rangi ya dark bluu nzito zenye color (zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 15,000/= kwa kila moja kwa atakayehitaji
viii. Gauni mbili za kijivu iliyokoza mshono wa solo za kushindia.
ix. Tai mbili za rangi ya dark bluu zenye mistari mieupe.
x. Tisheti moja yenye color ya mviringo ya rangi ya bluu kwa wote (inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 8,000/= kwa anayehitaji

### 2.2 Sare za shule kwa wavulana

i. Suruali mbili za bluu bahari zenye marinda mawili na mifuko mitatu zisizobana mwili ukubwa wa turn up inch 15 kwa Wavulana. Aina ya kitambaa ni cotton nzito namba 1.
ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu
iii. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
iv. Soksi jozi mbili nyeusi.
v. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
vi. Sweta rangi ya dark bluu yenye V shingoni.
vii. T-shirt yenye rangi ya dark bluu nzito zenye color (zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 15,000/= kwa kila moja kwa atakayehitaji
viii. Suruali mbili za rangi ya kijivu iliyokoza za kushindia
ix. Tai mbili za rangi ya dark bluu zenye mistari mieupe. Zinapatikana shuleni
x. Tisheti moja yenye color ya mviringo ya rangi ya kijani kwa wote (inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 8,000/= kwa atakayehitaji

### 2.3 Nguo za Michezo

i. Track suit ya dark bluu pea moja (yenye mistari mitatu mieupe mikononi)
ii. Bukta ya dark bluu moja
iii. Raba nyeupe na soksi nyeusi kwa wote.
iv. T-shirt moja ya rangi ya dark bluu yenye kola na isiyo na maandishi

### 2.4 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari ya kaunta zisizopungua kumi(10);
ii. **Ream (A4)** ya karatasi aina ya **double A** Mbili (2) kwa mwaka, moja kila muhula;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika angalau kitabu kimoja kwa kila somo.
iv. Scientific Calculator fx 991
v. **Dissection kit** – Kwa ajili ya upasuaji wa wanyama wadogo wadogo katika maabara (**CBG)**.
vi. **Laboratory coat** – Kwa ajili ya kuvaa wakati wa mazoezi ya maabara kuzuia madhara ya kemikali kwa tahasusi ya **CBG tu.**
vii. Godoro moja inchi mbili na nusu kwa sita( 2 ½ x 6);
viii. Mashuka ya bluu Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1, mto 1 kwa wavulana na Mashuka ya pink Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 na mto 1 kwa wasichana.
ix. Nguo za ndani za kutosha;

x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xi. Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) na 1 kubwa (lita ishirini) zenye mifuniko;
xii. Fekeo 1, reki 1, mfagio laini 1 (soft broom), Mfagio 1 wa nje (chelewa) na dawa ya chooni lita 5 kwa wanafunzi wa **EGM**
xiii. Jembe 1 lenye mpini, mfagio 1 mgumu (hard broom), Squeezer 1, Mfagio 1 wa nje (chelewa) na dawa ya chooni lita 5 kwa wanafunzi wa **CBG**
xiv. File folder 1 la plastic
xv. Rulled paper Mbili (02) kwa muhula.
xvi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
xvii. Mwanafunzi mwenye bima ya afya ya NHIF aje nayo shuleni.
xviii. Kwa mwanafunzi ambaye hana bima ya afya Mzazi/Mlezi ni lazima kuchangia kiasi cha shilingi Elfu hamsini na mianne (50,400/=) kwa ajili ya kukatiwa bima ya afya atakayoitumia kwa ajili ya matibabu yake awapo shuleni. Pesa hii inalipiwa ofisini,tafadhali isiwekwe benki.
xix.

## 2.2 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule bank ya **NMB** akaunti numba **30301200329** jina **MUGANGO SECONDARY SCHOOL.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MUGANGO**

**Wako,**

**ERNEST NCHUNGILWA MAZOYA**
**MKUU WA SHULE MUGANGO SEKONDARI**

**MAWASILIANO:**

- **Mkuu wa shule:0753912357/0679912357/ Email: mazoya.e@gmail.com**
- **Makamu Mkuu wa Shule:0759287828**
- **Mwandamizi Taaluma: 0688293859**
- **Mwandamizi Malezi na nidhamu: 0685156048**

**SHULE YA SEKONDARI MUGANGO**

**FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

i. JINAKAMILILAMWANAFUNZI:________________________________________________

ii. TAREHEYAKUZALIWA:________________KABILA_______________DINI_______________

iii. SHULE ALIYOTOKA:___________________________________________

iv. MWANAFUNZI ANATOKA MTAA WA/KIJIJI CHA__________________________

v. KATA YA:____________________TARAFA YA_______________________

vi. WILAYA YA_____________________MKOA WA:_____________________

vii. WAZAZI WOTE WAPO HAI/MMOJA YU-HAI/YATIMA (FUTA ISIYOHUSIKA)

viii. JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI_____________________________________

ix. KAZI YA MZAZI/MLEZI_____________________KAMA MLEZI TAJA UHUSIANO____________

x. ANUANI YA MZAZI/MLEZI________________________SIMU___________

1. Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.

2. Nitahakikisha na ninaahidi kuhudhuria darasani siku zote za masomo.

3. Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile pindi nikiwa mwanafunzi hapa Mugango sekondari. Naahidi nitadumisha nidhamu nzuri hapa shuleni.

4. Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.

5. Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakapoenda kinyume na sheria za shule.

**JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………… TAREHE………………………………….**

## FOMU YA AHADI YA MZAZI WA MWANAFUNZI

JINA LAMZAZI/MLEZI_____________________________________________

i. Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na sheria za shule ya sekondari Mugango aliyopewa mwanangu na ninakubaliana nayo.

ii. Ninakubali nafasi aliyopewa mwanangu.

iii. Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yake yote muhimu ya shule.

iv. Nitakuwa bega kwa bega na walimu katika kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata sheria na kanuni zilizo shuleni. Ni dhamu nzuri ya mtoto ndiyo mafanikio yake.

v. Naahidi kuwa mwanangu hatashiriki mgomo,fujo na wala makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyoahidi. Ikitokea akikiuka hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

vi. Tafadhali jaza majina, namba za simu na kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ndugu/jamaa na mwanafunzi watakaokuja shuleni kumtembelea au kuwasiliana nae kwanjia ya simu kupitia uongozi wa shule.

| S/N | JINA | UHUSIANO | NA. SIMU | ANAKOISHI | KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

------------------------------- -------------------------------

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** **TAREHE**

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI …………………………………………..

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

MUGANGO SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 1355,
**MUSOMA.**

25/04/2026

The Medical Officer,
……………………………..

RE: ……………………………………………………………(Full name of student).

Please kindly examine the above named as to his/her Physical and mental for enrolment as a student, the examination should include the following categories.
1. (a)Eye–Sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Venereal diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy.
2. Neurosis.
3. Pregnancy.
4. Other serious diseases.

**THE HEADMASTER**

**PART B MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a government Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNIFIT for fulltime of schooling.

1. (a) Eye–Sight……………………………………………………….
   (b)Hearing……………………………………………………………………….
   (c)Limbs………………………………………………………………………….
   (d)Speech………………………………………………………………………..
   (e)Venereal diseases…………………………………………………………….
   (f)Leprosy………………………………………………………………………..
   (g)Epilepsy……………………………………………………………………….
2. Neuroses……………………………………………………………….
3. Pregnancy………………………………………………………………………….
4. Other serious diseases…………………………………………………………….

Date …………… Signature ……………………… Station ……………………… Designati…………………………………………………………………………..